

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA



Hospitali ya Rufaa ya Mkoa
Musoma
S.L.P 21,
01 Barabara ya Mukendo,
31101-Musoma Mara.

Kumb.Na: DC.12/52/01/144

20 Juni, 2023

TANGAZO LA NAFASI YA KUJITOLEA

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Musoma - Mara, inatangaza nafasi za kujitolea kwa Kada mbalimbali kwa muda wa miezi kumi na mbili (12) kama ifuatavyo:-

NA.	KADA	IDADI YA NAFASI
1.	DAKTARI DARAJA II	5
2.	MFAMASIA	2
3.	KATIBU WA AFYA	1
4.	AFISA MUUGUZI	4
5.	AFISA MUUGUZI MSAIDIZI	9
6.	WAS Aidizi wa Afya	11
7.	WATEKNOLOJIA DAWA	5
8.	WATEKNOLOJIA MIONZI	3
9.	WATEKNOLOJIA MAABARA	2
10.	AFISA TAKWIMU DARAJA LA II	1
11.	KARANI WA TAKWIMU (DATA CLERK)	6
12.	AFISA HESABU DARAJA II	3
13.	AFISA HESABU MSAIDIZI	3
14.	AFISA MAPATO MSAIDIZI	2
15.	AFISA UGAVI	2
16.	AFISA HABARI	1
17.	AFISA TEHAMA	2
18.	AFISA USTAWI	2
19.	DOBI	3
20.	DEREVA	4
21.	FUNDI UMEME	1
22.	WATUNZA CHUMBA CHA KUHFADHI MAITI	3

A. SIFA ZA JUMLA KWA KADA ZA AFYA:

Waombaji wanatakiwa kuwa na;

- (i) Cheti cha taaluma cha Kada aliyosomea cha Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- (ii) Awe amemaliza mafunzo ya kazi (Internship) kwa Kada za Udaktari, Famasia na Afisa Muuguzi.
- (iii) Awe amesajiliwa na Baraza la Kitaaluma kwa Kada za Afya.
- (iv) Awe na Leseni ya taaluma husika.

B. SIFA ZA JUMLA KWA KADA ZISIZO ZA AFYA:

Waombaji wanatakiwa kuwa na;

- (i) Cheti cha taaluma cha kozi aliyosomea cha Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- (ii) Cheti cha Usajili wa Bodi ya kitaaluma kwa kada za Manunuzi na Ugavi.
- (iii) Kwa nafasi ya Karani wa takwimu (Data Clerk) anatakiwa awe na cheti cha Stashahada katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Tehama, Rasilimali watu, Sheria, Kumbukumbu za Afya na Ustawi wa Jamii katika Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na ujuzi wa Kompyuta.

3.0 MASHARTI YA JUMLA YA WAOMBAJI:

Waombaji wote wanatakiwa kuwa na sifa za jumla kama ifuatavyo:-

- (i) Awe raia wa Tanzania;
- (ii) Awe na umri usiozidi miaka 45;
- (iii) Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea (Cheti cha Kidato cha Nne, Sita, Taaluma na Usajili kamili) "Full Registration" au Leseni hai ya kufanya kazi ya taaluma husika.
- (iv) Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- (v) Maombi yaambatane na wasifu wa mwombaji (CV).
- (vi) Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma na Cheti cha kuzaliwa.
- (vii) Testimonials result slips **HAITAKUBALIWA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 06/07/2023.

Maombi yatumwe kwa:-

**Mganga Mfawidhi,
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Musoma - Mara,
S.L.P 21,
MUSOMA.**

Imetolewa na;



**Dkt. Osimund J. Dyegura
MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MUSOMA – MARA**

